# Karibu Kwenye Mwaka Wa Shule Wa 2024-2025
# Idara ya Huduma za Chakula na Lishe ( Food & Nutrition Services)

Jerranetta Brookings, Mkurugenzi mteule wa Food & Nutrition Services, **(314) 345-2320 x72320**
Tenecia Williams, Mtaalam wa Uwajibikaji **(314) 345-2308 x72308**
Karen Lee, Mtaalam Upishi **(314) 331-6115 x 76115**

---

Hamjambo Wazazi/Walezi:

Kwa niaba ya Idara ya Huduma za Chakula na Lishe ya shule zote za umma za Saint Louis (Saint Louis Public Schools, SLPS) tafadhali niruhusu niwakaribishe kirasmi ninyi na wanafunzi wenu kwa mwaka wa shule wa 2024-2025.

Shule za Umma za Saint Louis (SLPS) zingependa kuanzisha Huduma ya Ubora wa Chakula ya Chartwells kama Kampuni ya Usimamizi wa Chakula Chartwells. Huduma ya Ubora wa Chakula ya Southwest itatoa huduma za usimamaizi katika migahawa ya shule.

Saint Louis Public Schools (SLPS) na Chartwells wanaamini ya kwamba moja wapo ya njia muhimu zaidi ya kuwasaidia wanafunzi kufanya vyema katika madarasa yao ni kuwapa chakula chenye afya bora na lishe kamilifu wanapokuwa shuleni.

**<u>Mpango wa Ustahiki Kushusu Utoaji Kwa Jamii:</u>**
Saint Louis Public Schools zinaendesha Mpango wa Ustahiki Kushusu Utoaji Kwa Jamii, jambo linaloruhusu wanafunzi wote wa shule za SLPS kupata kiamshakinywa, chakula cha mchamchana, kilalio na kitafunio bila malipo.

**Idara ya Huduma ya Chakula na Lishe ya SLPS inatekeleza Mipango ya Lishe ya Watoto ifuatayo ambayo inafadhililiwa na Idara ya Kilimo ya Marakani (Federal Child Nutrition Programs sponsored by the United States Department of Agriculture, USDA), Idara ya Elimu ya Msingi na Sekondari (Department of Elementary and Secondary Education, DESE), na Huduma Kuu za Idara na Afya za Missouri**

- Mpango wa Shule Kuhusu Kiamsha Kinywa (School Breakfast Program, SBP)
- Mpango wa Shule Kuhusu Chakula cha Mchamchana (National School Lunch Program, NSLP)
- Mpango wa Matunda na Mboga (Fresh Fruit and Vegetable Program, FFVP)
- Mpango wa Kitafunio cha Alasiri (Afterschool Snack Program, ASP)
- Vitafunio Mahiri/Vichangisha fedha
- Mpango wa Huduma ya Chakula kwa Watoto na Watu Wazima (The Child and Adult Care Food Program, CACFP)
- Mpango wa Chakula cha Majira ya Joto (Summer Food Service Program, SFSP)

**<u>Mpango wa Shule Kuhusu Kiamshakinywa:</u>**
- Kiamshakinywa ni bila malipo kwa wanafunzi wote. **Watu Wazima Wanalipia Chakula: <u>$2.84.</u>**
- Chakula kinahudumiwa kabla ya shule kuanza katika madarasa (pk-k) na migahawani.
- Chaguo la Chakula moto (hot entrée) nafaka, tunda au sharubati ya 100%, maziwa ya kiwango cha chini cha 1% ya mafuta au maziwa yasiyo na mafuta kabisa.
- **Maziwa yoyote ya ziada yanaweza kununuliwa: meupe - $.60 chokolate: -$.65.**
- Menyu ziko kwenye tovuti ya Saint Louis Public Schools (www.slps.org/menus).

**Mipango ya Shule Kuhusu** Chakula cha Mchamchana**:**

***Shule za Msingi*:**

- Chakula cha Mchamchana ni bila malipo kwa wanafunzi wote. **Watu Wazima Wanalipia Chakula**: **$5.29.**
- Chakula cha Mchamchana kinajumuisha chaguo la Chakula moto (hot entrees), vyakula vya nafaka nzima, mboga, walaji mboga
  chaguo la chakula, na 1% ya maziwa yaliyo na kiwango cha chini cha mafuta au maziwa ya chokoleti yasiyo na mafuta.
- Vyakula vinahudumiwa madarasani (pk-k) na migahawani.
- **Maziwa yoyote ya ziada yanaweza kununuliwa : meupe- $.60 chokoleti- $.65.**
- Menyu ziko kwenye tovuti ya Saint Louis Public Schools (www.slps.org/menus).
- Kila mwanafunzi atabonyeza enter kwenye kicharazio cha vitufe cha Kifaa cha Mauzo (Point of Sales, POS) anapopokea kiamshakinywa au chakula cha mchamchana.

***Shule za Kati na Upili:***

- Chakula cha Mchamchana ni bila malipo kwa wanafunzi wote. **Watu Wazima Wanalipia Chakula: $5.29.**
- Chakula cha Mchamchana kinajumuisha Vyakula moto vyenye afya (hot entrees), vyakula vya nafaka nzima, machaguo mbadala ya chakula cha walaji mboga, na 1% ya maziwa yaliyo na kiwango cha chini cha mafuta au maziwa ya chokoleti yasiyo na mafuta kabisa.
- **Maziwa yoyote ya ziada yanaweza kununuliwa: Meupe- $.60 chokoleti- $.65.**
- Eneo la Matunda na mboga mbichi kwa ajili machaguo ya ulaji wenye afya.
- Menyu ziko kwenye tovuti ya Saint Louis Public Schools (www.slps.org/menus).
- Kila mwanafunzi atatumia kicharazio cha Point of Sales (POS) kuweka nambari Binafsi ya Utambulisho (Personal Identification Number, PIN) wakati wa kupokea kiamshakinywa na chakula cha mchamchana. PIN itabaki ileile kila mwaka.

**Mpango wa Huduma ya Chakula kwa Watoto na Watu Wazima (The Child and Adult Care Food Program, CACFP): Mpango wa Kilalio cha Baada ya Shule**

- Mpango wa Baada ya Shule wa Idara ya Afya na Huduma Kuu ya Missouri.
- Wanafunzi wanapewa kilalio na vitafunio vilivyo na lishe bora.
- Shule zinazotoa mpango wa baada ya shule unaojumuisha, elimu, lishe bora, na mipango ya michezo zinastahiki kushiriki.
- Shule zinaweza kupokea chakula cha milo baridi au moto.

**Taaarifa ya Ziada Kuhusu Lishe:**

- Tembelea tovuti ya SLPS: www.slps.org.
  - Ili kutathmini muhtasari wa Idara ya Huduma ya Chakula na Lishe, nenda kwa: www.slps.org, bonyeza kwenya **Kichupo cha Wazazi na Wanafunzi (Parent & Student Tab),** Kisha nenda kwa **Muhtasari (Overview).**
  - Ili kutathmini **Sera ya chakula na Menyu na Barua za Ukaribisho wa Wazazi** katika lugha za zingine**, nenda kwa** www.slps.org, bonyeza kwa **Parent & Student Tab,** Kisha nenda **Sera ya Chakula na Menyu (Meal Policy and Menus).**
  - Ili kutathmini Sera ya Afya na Ustawi au kutazama Sera katika lugha nyingine, nenda kwawww.slps.org, bonyeza kwa **Parent & Student Tab,** kisha nenda kwa **Afya na Ustawi (Health and Wellness).**
  - Ili kutathmini **taarifa kuhusu nambari ya utambulisho wa kibinafsi (PIN), nenda kwa** www.slps.org, bonyeza kwa **Parent & Student Tab,** kisha nenda kwa **Meal Policy and Menus**.

Tafadhali wasiliana na Idara ya Huduma ya Chakula na Lishe kwa (314) 345-2308 ikiwa una maswali yoyote.

Tena, Ningependa kuwashukuru kwa ajili ya Msaada na Usaidizi wenu mwaka huu.

*Jerranetta Brookings*

Mkurugenzi mteule Huduma za wa Chakula na Lishe

**Taasisi hii ni mtoahuduma wa fursa sawa.**

# OMBA TAARIFA

**(Jaza fomu moja kwa kila jamii)**

Tafadhali jibu maswali yaliyo hapo chini kwa kuchagua kisanduku kinachofaa. Taarifa ifuatayo ni ombi ambalo liliafikiwa na Kongamano Kuu katika mwaka wa 2010 likihitaji jumuia ya shule kubaini ikiwa watoto wote katika familia wana bima ya afya.

Je, kila mtoto katika familia yako ana bima ya afya?

☐ NDIO

☐ LA

**MO HealthNet (Medicaid) inazingatiwa kama bima ya afya.**

Ikiwa La itachaguliwa jumuia ya shule itatoa swali la Je, Mtoto wako Anahitaji Fomu ya Usimamizi Huduma ya Bima ya Afya kwa Ajili ya Familia.

Kujaza fomu hii siyo hali  ya kubaini ustahiki wako wa kupata chakula.  Ombi la Chakula cha Bure na Kilichopunguzwa Bei litakaguliwa bila kujali jibu lako kwa Ombi la taarifa.

Rudisha fomu hii iliyojazwa shuleni/ jumuia ya shule.

Jina lililochapishwa la mzazi/mlezi: ______________________________

Anwani ya Barua ya Posta: ______________________________

Jiji: ____________________ Jimbo: __________ Nambari Maalum ya Posta: __________

Idara ya Elimu ya Shule ya Msingi na Sekondari haibagui kwa misingi ya asili ya taba ya mbari, rangi, dini, jinsia, asili ya kitaifa, umri, au ulemavu katika mipango na shughuli zao.  Maswali kuhusu mipango ya Idara, na maeneo ya huduma, shughuli, na vifaa vinavyofikiwa na watu walio na ulemavu vinaweza kuelekezwa katika Jefferson State Office Building, Office of the General Counsel, Coordinator – Civil Rights Compliance (Title VI/Title IX/504/ADA/Age Act), 6th Floor, 205 Jefferson Street, P.O. Box 480, Jefferson City, MO 65102-0480; simu 573-526-4757 au TTY 800-735-2966; baruapepe civilrights@dese.mo.gov.

Saint Louis Public Schools    801 N. 11th Street    St. Louis, MO 63101    314-345-4519